**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**
**Mkuu wa Shule :0653812859**
**0767989595**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0753979204**
**Patron:0787003468**
**Msajili: 0769894026**
**Shule ya Sekondari Nyamunga**
**S.L.P 1295**
**Tarehe 12/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYAMUNGA HALMASHAURI YA RORYA MKOA MARA MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Nyamunga ipo umbali wa Kilometa 11 kutoka musoma hadi shuleni. Usafiri wa basi kutoka mjini Mwanza unapatikana katika kituo cha mabasi Nyamongoro(uliza Basi Johamvia-Ndio mzee inayoenda Kibuyi) Nauli ni Shilingi 12,000/= ushuke kibao cha Nyamunga Sekondari na ufate maelekezo ya kibao hicho au ukitoka mwanza shuka Musoma stendi ya Bweri panda daladala hadi stendi ya zamani Musoma mjini nauli Tsh 500/=, chukua usafiri wa bodaboda hadi kivukoni Mwigobero Tsh 1000/= kisha panda feri ya Musoma –Kinesi Tsh 400/=. Ukifika kinesi kuna usafiri wa bodaboda Tsh 2000/= au kwa miguu mpaka shuleni

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30/06/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Suruali (1) rangi ya kijivu (rangi ya kitambaa namba 02), marinda mawili pande zote, mifuko mitatu (mmoja wa nyuma na miwili ya mbele) mguu 16cm iwe na turnup/iwe na upinde chini aje nayo.
ii. Suruali (1) rangi ya dark blue (rangi ya kitambaa namba 01) yenye marinda mawili pande zote. Mifuko mitatu (mmoja wa nyuma na miwili ya mbele) mguu 16cm iwe na turnup/iwe na upinde chini aje nayo.
iii. Shati mbili au Zaidi nyeupe za MIKONO MIREFU na zenye mfuko mmoja tu aje nayo.
iv. T-shirt mbili (02) rangi ya blue moja(1) na rangi ya kijivu moja (1) yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 12,000/= kwa T-shirt moja.
v. Sweta moja la kuvaa (special) wakati wa baridi rangi ya kijivu namba 01 yenye nembo ya shule (inaweza kupatikana jirani na shuleni) kwa Tsh 15,000/=
vi. Viatu vya ngozi nyeusi vya Kamba jozi mbili (02) na visiwe na visigino virefu wala muundo wa (boot) aje navyo.
vii. Soksi nyeusi jozi (04) na zisiwe na mistari au madoadoa . aje nazo.
viii. Mkanda mweusi wa kiume (upana inchi 1.5) kufungia suruali. Aje nao.
ix. Viatu vya raba za michezo na shughuli za nje. Aje navyo.
x. Track suit nyeusi/blue. Yenye nembo ya shule (inaweza kupatikana jirani na shuleni) kwa Tsh 25,000/=
xi. Suruali (02) za kushindia za rangi nyeusi na kaki iwe na marinda mawili(02) pande zote mbili, mguu 16cm ( ndio avae siku ya kuripoti, asije kabisa na nguo ya nyumbani)
xii. Tai mbili (02) rangi ya kijivu na nyingine dark blue. Aje nazo.
xiii. Koti la maabara jeupe litavaliwa wakati wa mafunzo kwa vitendo kwa PCB na CBG (aje nalo)
xiv. Dissecting kit moja kwa tahasusi ya PCB na CBG moja (01) (aje nayo)

NB:

- Nguo zote za kiraia haziruhusiwi kabisa kuonekana wala kuvaliwa shuleni, hivyo basi mwanafunzi asije nazo shuleni kabisa
- Siku ya kuripoti aje amevaa sare za shule (shati Nyeupe na suruali ya kijivu au ya Blue)
- Shule haina huduma ya kupiga mihuri kwa mwanafunzi mmoja mmoja hivyo mwanafunzi anashauriwa kununua sweta, truck suits na t-shirts zikiwa na mihuri

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftali Makubwa Counter Book quire 3 au 4 Yasiyopungua saba 7 na pia daftali Ndogo za Mazoezi zisizopungua (07)
ii. Pesa ya huduma ya kwanza Tsh 5,000 (aje nayo mkononi)
iii. Bima ya afya (kwa asiyekua na bima ya afya anatakiwa aje na Tsh 5,000 kwa ajili ya kukatiwa Bima ya Afya ya wanafunzi)
iv. **Ream aina ya DOUBLE A (A4)** ya Karatasi nne (4) kwa mwaka zinaweza patikana kwenye duka la shule kwa tsh 17000/=;
v. Graph Pad Pisi 5.

vi. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vilivyoandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE);
vii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
viii. Scientific Calculator fx 991 kwa wanafunzi wa PCB na CBG (Origino zinapatikana kwenye duka la shule kwa tsh 30,000/=);
ix. Godoro la sponge la upana wa futi 2.5×6 linaweza patikana kwenye duka la shule kwa bei ya tsh 35000.
x. Dawa ya kusafishia choo lita 5
xi. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*Rangi ya blue);*
xii. Nguo za ndani za kutosha;
xiii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) vinaweza patikana kwenye duka la shule;
xiv. Ndoo 1 kubwa (lita ishirini) yenye mifuniko (kwa ajili ya matumizi ya shule);
xv. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) yenye mifuniko (kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi);
xvi. Squizer 1, hard broom 1, soft broom 1, Kwanja 1, jembe 1, mfagio wa chelewa wenye mpini kwa ajili ya nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi | maelekezo | NAMBA YA ACCOUNT NMB |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= | Iwekwe benki | 30401200109 NYAMUNGA SECONDARY SCHOOL RECURRENY ACCOUNT |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= | Aje nayo mkonononi | |
| 4. | Nembo | 5,000/= | Aje nayo mkonononi | |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= | Aje nayo mkonononi | |
| | **Jumla** | **80,000/=** | | |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ……………………………

**Jina la Mkuu wa Shule: Patrick M. Wadugu**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:** 


**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0653812859/0767989595**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0753979204**
- **Mwandamizi Taaluma: 0765301351**
- **Mwandamizi Malezi: 0758252463**
- Msajili: 0769894026

HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA SHULE VA SEKONDARI NYAMUNGA
HISTORIA/TARIFA YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili (kama linavyoonekana kwenye result slip au school leaving certificate)………………………………………………………………………………………

2. Mahali mwanafunzi Alipozaliwa Mtaa wa………… kijiji cha………kata ya………………Wilaya ya…………Mkoa..................

3. Dini…………………Dhehebu………………………

4. Unaingia Kidato cha ............................. Tarehe/Mwaka ..................

5. kutoka shule ya Sekondari……………Wilaya……………...Mkoa……………

6. Usafiri Kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni (Toa maelezo)
i)………………………………………………………………………………………
ii)………………………………………………………………………………………

7. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala ya shule:

| SN | JINA | PICHA | UHUSIANO | KAZI | ANUANI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| I. | | | **BABA** | | | |
| II. | | | **MAMA** | | | |
| III. | | | **MLEZI (1)** | | | |
| IV | | | **MLEZI(2)** | | | |

8. Kabla ya kuripoti hapa shuleni umepimwa na daktari? Ndiyo/Hapana ni ugonjwa upi ni wa kudumu kwako? ...........................................................................

9. Sifa maalumu kama unazo .....................................................................

10. Unalipiwa/Utalipiwa Karo na (Taja jina anwani yake na namba zasimu) …………………………

11. Tarifa za Wazazi wako kama Wapo…………Wamefariki…… (Weka alama ya vyema panapohusika)

Nakiri kuwa maelezo yaliyopo hapo juu ni sahihi.

......................... …………………………

SAINI YA MWANAFUNZI SAINI YA MZAZI/MLEZI

AHADI YA MWANAFUNZI

MIMI

(Jina la mwanafunzi)…………………………………….……..…nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii.Naahidi kufuata sheria za shulena taratibu zote zilizotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

AHADI YA MZAZI/MLEZI:

MIMI(Jina)………………………………………………………………………Ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………………………………….nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Nyamunga ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia mwema wa Taifa letu

Jina la mzazi/mlezi………………………….. jina la mwanafunzi…………………………….

Saini ya mzazi/mlezi……………….. saini ya mwanafunzi…………………..

Tarehe…………………… Tarehe…………………….…

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL ADMINISTRATIONS**
**NYAMUNGA SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

*(To be filled by an Authorized Government Medical Officer)*

Full name of Student …………………………………………………………….
Age ……………………
Height (in cms) …………………………………… Weight (in kgs)………………………………….

1. Blood count ………………………… (Red and White) ……………………………
2. Stool Examination ……………………………………………………………………
3. Urine analysis ………………………………………………………………………….
4. Syphilis and other V.D ………………………………………………………………
5. T.B. and Leprosy Test ……………………………………………………………….
6. Eye Test …………………………………………………………………………….
7. Ear Test ………………………………………………………………………………
8. Chest Test ……………………………………………………………………………
9. Abdominal Test …………………………………………………………………….
10. Blood Group (very crucial) ……………………………………………………
11. Spleen……………………………………………………………………………
12. H.I.V. Test, Positive ………☐………… Negative …☐…………
    (Tick where necessary)

Additional information e.g. Physical defects or impairment, infections, chronic or family Diseases (eg Sickle cell)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

I (full name) …………………………………………………………… Certify that the above student is fit/is not fit pursue Secondary Education.

Designation ………………………………………

Station ……………………………………………… Signature ……………………………………

Date……………………………………………… Rubber Stamp